

Je ni kweli?

KUANGALIA UKWELI KUHUSU CHANJO YA COVID-19

1 Chanjo ya COVID-19 HAITABADILISHA jeni (kitengo cha msingi cha urithi) yako au molekuli kubwa ndani ya seli za viumbehai (DNA.)

Chanjo zote mbili za Moderna na Pfizer zinatumia mRNA. Kiini/dutu inayozalishwa na miili yetu kiasili. mRNA inafundisha miili yetu kutukinga kwa kutengeneza kingamwili na seli nyingine zinazopambana na maambukizi.

mRNA kutoka kwa chanjo ya COVID-19 kamwe haiingii kwenye kiini cha seli -ambapo molekuli kubwa ndani ya seli za viumbehai (DNA) huhifadhiwa. Hii inamaanisha kuwa mRNA haiwezi kuathiri molekuli kubwa ndani ya seli za viumbehai (DNA) kwa namna yoyote. Mara tu mRNA ikimaliza kufunza seli zetu, molekuli ya protini ambayo hufanya kazi kama kichocheo cha kibayolojia huvunja mRNA kwa hivyo haipo tena katika miili yetu.

Je chanjo ya COVID inawezabadilisha molekuli kubwa ndani ya seli za viumbehai (DNA) katika mwili wangu? Tabia zangu za kipekee? Jeni (kitengo cha msingi cha urithi) kwa familia yangu?



2 Chanjo ya COVID-19 haitakuambukiza virusi vya korona.

Hakuna virusi vya korona kwa chanjo yoyote ya COVID-19. Huwezi kupata virusi vya korona kutokana na kupokea chanjo.

Chanjo hii hufundisha seli za miili yetu kutengeneza protini inayofanana kabisa na ile inayopatikana juu ya virusi vya COVID-19. Ili kutoa maagizo, chanjo hii hutumia aidha, mRNA au virusi vya homa ya kawaida visivyokuwa na madhara ambavyo hubadilishwa ili visiweze kusababisha ugonjwa. Miili yetu hujifunza kutambua protini hiyo ili iweze kuweka majibu ya kinga ikiwa virusi vya COVID-19 vitaingia mwilini.

Je naweza kupata ugonjwa wa COVID-19 kutoka kwa chanjo?



3

Chanjo za COVID-19 zinaweza kusababisha dalili kama za homa ambayo si kali, Lakini athari kali ni nadra sana.

Inawezekana kupata athari kama maumivu ya kichwa, kuvimba mkono, uchovu au joto jingi mwilini siku moja au mbili baada ya kupata chanjo. Lakini athari hizi hazidumu kwa muda mrefu na ni ishara kwamba chanjo inafanya kazi.

Athari kali za mzio (anaphylaxis) ni nadra sana, lakini inaweza tokea, hasa kwa watu walio na hali mbaya ya mzio. Zote zinatibika.

ulinzi umewekwa, ikiwa tu utahitajika. Baada ya kupata chanjo, utaulizwa kusubiri katika kliniki kwa dakika kumi na tano ili kuhakikisha kuwa hauna athari kali ya mzio kwa chanjo.



Nina wasiwasi juu ya kuwa na athari mbaya za mzio kwa chanjo ya COVID-19

4

Chanjo za COVID-19 hazina chipu/kifaa cha kufuatilia mtu au kitu, tishu za kijusi, bidhaa za nguruwe, vyuma hatari au viungo vyenye sumu.

Nimesikia uvumi mwingi kuhusu kile ambacho kimo kwenye chanjo.

Kiungo muhimu katika chanjo zote za Pfizer na Moderna ni nyenzo ya maumbile itwayo mRNA. Chanjo hizi pia zina lipidi, chumvi, asidi asetiki (kiungo kikuu cha siki), na sukari. Katika chanjo ya Johnson & Johnson (J&J), kiungo muhimu ni virusi vya homa ya kawaida, vilivyobadilishwa ilivisiweze kusababisha ugonjwa. Chanjo ya J&J pia ina vidhibiti (chumvi, mvinyo, polysorbate 80, asidi hidrokloriki) na asidi za amino. Chanjo hizi zina viungo vichache kuliko mfuko wa wastani wa vibanzi vya viazi!



5


Chanjo ya COVID-19 itapunguza watu kulazwa hospitalini na vifo katika jamii za watu wenye rangi.

Kabla ya chanjo za COVID-19 kutengenezwa, wanaharakati na mawakili waliibua wasiwasi kuhusu madhara yanayoendelea ya kihistoria yanayosababishwa na taasisi za matibabu na serikali kwa watu weusi, wenyeji, na watu wa rangi. Shukrani kwa juhudi zao, maelfu ya watu walioshiriki katika majaribio ya chanjo ya COVID-19 inaashiria utofauti wa idadi ya watu wetu. Chanjo hizi zimekuwa na ufanisi na ni salama katika kabila na makundi ya makabila.



kwa kuongezea, watu wenye rangi walitekeleza majukumu ya uongozi katika ukuzaji/utengenezaji wa chanjo, kwa mfano Dkt. Kizzmekia Corbett, mwanasayansi mweusi ndiye anayeongoza taasisi ya kitaifa ya afya inayohusika na utafiti kuhusu chanjo ya virusi vya korona

Watu weusi, wenyeji wa marekani, walatino, na jamii ya watu wa kisiwa cha pasifiki wamepata viwango vya juu zaidi vya watu kulazwa hospitalini na vifo kutokana na COVID-19 katika kaunti ya King. Jamii hizi zitakuwa kati ya jamii ambazo zitafaidika zaidi na kinga ambayo chanjo inatoa.



Rasilimali za ziada



Kwa maelezo zaidi kuhusu chanjo ya COVID-19 na kubaini ikiwa unastahiki kupata chanjo: Tembelea tovuti ya: kingcounty.gov/vaccine



Jifunze kuhusu kujitunza ukiwa na COVID-19, kupimwa, kujitenga/karantini, na rasilimali kwa mashirika: Tembelea tovuti ya: kingcounty.gov/covid



Kwa maswali ya matibabu ya COVID-19 au usaidizi wa kupanga jinsi unaweza kupimwa COVID-19 au kujisajili ili upate chanjo, piga simu kwa nambari: (206) 477-3977 siku yoyote kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa moja usiku. Wakalimani wanapatikana.